


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI NA TATU



26 JUNI, 2019

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI NA TATU – TAREHE 26 JUNI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 [*The Finance Bill, 2019*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:

Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 [*The Finance Bill, 2019*].

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 [The Finance Bill, 2019].

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

459. MHESHIMIWA FRANK GEORGE MWAKAJOKA (TUNDUMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itasimamia na kuhakikisha Madereva wa Malori na Mabasi wanapata Mikataba ya Ajira ili kuboresha maslahi yao na kuongeza ufanisi katika utumishi wao.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

460. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS GULAMALI (MANONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya ya Igunga ilipata ufadhili wa Benki ya Dunia wa ujenzi wa Vituo vya Afya vya Simbo, Ziba, Choma cha Nkola na Igurubi ambapo Vituo vya Afya vya Ziba, Choma cha Nkola na Igurubi vimekamilika na vifaa tayari viro japo majengo na vifaa katika Kituo cha Afya cha

Choma cha Nkola na Igurubi bado havijaanza kufanya kazi; Kituo cha Afya cha Simbo bado hakijakamilika na vifaa havipo na Wafadhili walishakabidhi Halmashauri bila kukamilisha ujenzi huo:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kujua nini kilicho jificha juu ya mradi huo kukabidhiwa bila kukamilika.

461. MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mji wa Kibaha unakuwa kwa kasi hivyo mahitaji ya Watumishi yameongezeka ikiwemo Watendaji wa Mitaa, Maofisa Mifugo, Walimu pamoja na Watumishi:-

Je, ni lini Serikali itatoa kibali cha ajira na kuajiri Watumishi pungufu ili kuleta ufanisi zaidi katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

462. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE (MPWAPWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali ilikuwa na mpango wa kufanya matengenezo makubwa barabara ya kutoka Mima kwenda Mkanana hadi Chibwegele; Mpango huo haujatekelezwa mpaka sasa:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza mpango huo ili barabara hiyo iweze kuitika wakati wote bila matatizo kuliko ilivyo sasa.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

463. MHESHIMIWA YUSSUF SALIM HUSSEIN (CHAMBANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali inafaidikaje na rasilimali ya miti ya mikoko ilioanza katika ukanda wa Pwani ya Tanga mpaka Mtwara.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

464. MHESHIMIWA RICHARD MGANGA NDASSA (SUMVE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Wananchi wa Halmashauri ya Kwimba waliombwa kutafuta eneo la kujenga Chuo cha VETA ambapo eneo la ekari 60 lilishapatikana zaidi ya miaka 10 iliyopita na Serikali imekuwa ikiahidi kutenga fedha za ujenzi wa Chuo hicho:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa Chuo hicho.

465. MHESHIMIWA EDWARD FRANZ MWALONGO (NJOMBE MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Elimu ya ufundi ni muhimu sana kwa Vijana:-

- (a) Je, Serikali ipo tayari kubadili Shule moja ya Sekondari katika kila Halmashauri na kuifanya kuwa Shule ya Ufundi;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha Kozi za Ualimu wa Ufundi iliyokuwa ikitolewa na *Dar – Institute & Technology*.

WIZARA YA NISHATI:

466. MHESHIMIWA DKT. SHUKURU JUMANNE KAWAMBWA (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Kasi ya utekelezaji wa miradi REA III A Jimboni Bagamoyo ni ndogo:-

Je, ni lini miradi hiyo itakamilishwa katika Jimbo la Bagamoyo.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

467. MHESHIMIWA MARWA RYOBA CHACHA (SERENGETI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara inayojengwa kuunganisha Mkoa wa Mara na Arusha inasuasua sana, kwani tangu ilipoanza kujengwa mwaka 2013 mpaka leo hata km 50 zimeshindwa kukamilika:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani dhidi ya ukamilishaji wa barabara hii;
- (b) Je, ni lini Wananchi waliofanyiwa tathmini watalipwa fidia zao.

468. MHESHIMIWA JOYCE BITTA SOKOMBI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara itokayo Bunda kwenda Musoma Vijijini ili kuwapunguzia Wananchi wa Saragana,

Bugoji, Mabhui, Melaturu, Kangetutya na Kanderema adha ya kuzunguka kuitia Musoma Mjini.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

469. MHESHIMIWA VICTOR KILASILE MWAMBALASWA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Miaka ya karibuni Samaki aina ya Gege (Pelege) katika Ziwa Rukwa wamepungua na kudumaa na hii ni kutokana na uchimbaji wa dhahabu Wilayani Chunya na Songwe ambao mara nyingi ulihusisha Zebaki:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya utafiti katika Ziwa hili.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

470. MHESHIMIWA RITTA ENESPER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Hospitali ya Mkoa wa Iringa inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa

Nyumba kwa ajili ya Madaktari Bingwa na hivyo kusababisha Madaktari hao kuishi mbali na Hospitali:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali kutatua changamoto hiyo.

471. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Ndoa za utotoni ni tatizo kubwa katika jamii zetu hususan katika jamii zenye umaskini:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa Umma hasa katika maeneo ya Vijijini ili Wananchi wafahamu athari za kuozesha Watoto katika umri mdogo.



WIZARA YA MADINI:

472. MHESHIMIWA CHRISTOPHER KAJORO CHIZA (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:- Kumekuwa na dalili za upatikanaji wa madini ya Dhahabu katika Vijiji vya Kabingo, Ruhuru, Nyakayenzi, Nyamwilonge na Muhange Wilayani Kakonko na katika baadhi ya Vijiji uchimbaji umeanza:-

Je, Serikali inatoa ushauri gani kwa Vijana ambao wapo tayari kujishughulisha na uchimbaji wa madini.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4), Bill, 2019*].

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5), Bill, 2019*].

Muswada wa Sheria ya Serikali Mtandao wa Mwaka 2019 [*The e-Government Bill, 2019*].

V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(*Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu*)

Muswada ya Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 [*The Finance Bill, 2019*].

DODOMA
26 JUNI, 2019

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE